## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI AGOSTI, 2025 NA MWELEKEO KWA MWEZI SEPTEMBA, 2025.

**Dondoo za tathmini ya Agosti, 2025 na mwelekeo wa Septemba, 2025:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Agosti, 2025 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa hususan hali ya joto kwa mwezi Septemba, 2025 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Agosti, 2025 hali ya baridi ilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususani nyakati za usiku na asubuhi. Hali ya baridi zaidi ilijitokeza katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi.

ii. Vipindi vifupi vya mvua zilizoambatana na radi vilijitokeza katika maeneo machache ya Ziwa Victoria. Hata hivyo, ukanda wa pwani pamoja na nyanda za juu kaskazini mashariki vilipata vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache. Aidha, vipindi vya upepo mkali unaofikia kasi ya kilometa 40 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini.

iii. Kwa mwezi Septemba 2025, hali ya baridi inatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini hususani katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi ikiambatana na hali ya ukavu kwa ujumla. Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo ya mwambao wa pwani, ukanda wa Ziwa Victoria, na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki.

### 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI AGOSTI, 2025.


Katika kipindi cha mwezi Agosti, 2025 hali ya baridi ilijitokeza katika maeneo mengi nchini hususani nyakati za usiku na asubuhi. Hali ya baridi zaidi ilijitokeza katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi, ambapo kiwango cha chini zaidi cha joto cha nyuzi joto cha 4.2 °C kilirekodiwa katika kituo cha Igeri (Njombe) mnamo tarehe 5 Agosti 2025. Aidha, vipindi vya upepo mkali uliofikia kasi ya kilomita 40 kwa saa vilirekodiwa katika

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727B - 02/2023*

baadhi ya maeneo nchini, hususan ukanda wa pwani na maziwa makuu. Kwa upande mwingine, vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo machache ya ukanda wa pwani, ukanda za Ziwa Victoria na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Kiwango cha juu cha mvua cha milimita 59.4 kwa saa 24 kilichopimwa katika kituo cha Musoma mnamo tarehe 18 Agosti, 2025.




Kielelezo 1: Viwango vya joto la chini kwa vituo vya Uyole na Igeri kwa mwezi Agosti, 2025

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI SEPTEMBA, 2025

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2025, Joto la Bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kati la kitropiki ya Bahari ya Pasifiki. Hali ya joto la

bahari katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) inatarajiwa kuwa la chini ya wastani. Hali hii inatarajiwa kusababisha upepo wenye unyevu kutoka misitu ya Congo kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Aidha, kuendelea kuwepo kwa joto la bahari la juu ya wastani katika ncha ya kusini mwa Afrika inatarajiwa kupunguza kuvuma kwa upepo wenye ubaridi kutoka kusini na hivyo kusababisha vipindi vichache vya baridi zaidi nyakati za usiku katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Pwani.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2025

Kipindi cha mwezi Septemba 2025, maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuwa na hali ya baridi kiasi, na viwango vya chini zaidi vya joto vinatarajiwa kuendelea katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi. Aidha, ongozeko kidogo la joto linatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Vipindi vifupi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan ya ukanda wa pwani na maziwa makuu.
Kwa upande wa mvua, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache, hususan yale yalioko ukanda wa pwani, Ziwa Victoria na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 18 °C hadi 25 °C katika maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani. Kwa maeneo ya nchi kavu kati ya nyuzi joto 14 °C na 20 °C. Kiujumla, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 12 °C. Kwa ujumla, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi, huku vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa hususan katika maeneo ya miinuko.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 22 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 14 °C. Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. Kwa upande mwingine, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 8 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Aidha, hali ya baridi zaidi ya kiwango cha chini ya nyuzi joto 8 °C

inatarajiwa katika maeneo ya miinuko, ikijumuisha mkoa wa Njombe. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 15 °C hadi 24 °C katika maeneo mengi. Aidha, hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa katika maeneo mengi pamoja na vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 10 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 10 °C . Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI OCKTOBA, 2025

Katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2025 ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani, Ziwa Victoria na maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Hali hii inatarajiwa kuambatana na upungufu wa vipindi vya ubaridi.

## 2.4 USHAURI

Tahadhari za kiafya zichukuliwe ili kulinda jamii dhidi ya magonjwa yanayoweza kusababishwa na baridi, vumbi na matumizi ya maji yasiyo safi na salama. Kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi katika kipindi hiki, maji na malisho yanapaswa kutumika kwa uangalifu ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Septemba, 2025 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**